Asomo ya biblia

Masomo haya ya Biblia yamebuniwa kutumika kwenye vikundi vidogo vidogo, yanaweza kutoa utangulizi wa manufaa kwenye Ibada ambako masomo mbalimbali kutoka kwenye mwongozo yanapojadiliwa, chagua somo ambalo litahusiana na somo unalopanga kujifunza au ambalo linaelekeana na hali yako wakati wa masomo, tia moyo watu kutafakari kwenye kile wanachosoma, kujadili maana na vidokezo vya kile wanachojifunza na mwisho kuomba kwa pamoja juu ya yale waliyojifunza.

SOMO LA BIBLIA 1

Nia ya mungu juu ya miti

Miti inatajwa katika mwisho wa Biblia na kufanya madaraka ya maana katika hali zote.

Soma Mwanzo 2:8-9.

- Je, Mungu anaichukuliaje miti? Soma Ufunuo 22:1-2
- Kwa nini unafikiri Mungu alichagua mti kuelezea uzima wa milele?

Mti huu unaonyesha mfano wa ukamilifu wa neema ya Mungu inayookoa katika Yesu Kristo. Ni furaha ya jinsi gani tunayo kwamba ilikuwa kwenye mti mwingine – msalaba – kwamba dhambi yetu (ambayo ilianza na Adamu na Hawa za kutomtii Mungu na kuchuma tunda kutoka kwenye mti waliokatazwa) ili samehewa.

SOMO LA BIBLIA 2

Miti na nyakati ngumu

Soma Kumbukumbu 20:19-20

- Je, ni amri zipi zinazotolewa hapa juu ya matumizi ya miti wakati wa vita?

Katika vita sheria za uzima zinabadilika, watu wanaweza kusahau pendo katika njia ile ile. Mazingira nayo yanateseka, katika siku zile, miti ilikatwa kwa matumizi katika kuteka miji ya adui. Mungu asingeweza kukataza kama vita wakati mwingine isingeepukika, badala yake yeye alijaribu kuzuia uharibifu unaousababishwa na vita, hivyo miti ya matunda isingekatwa, kwa nini, kwa sababu hii halikuwemo katika faida zao za baadaye. Hakuna miti ya matunda ina maana kuwa hakuna tunda, chakula kidogo na watu wenye njaa. Hapa ni mafundisho dhahiri kwamba hatuna haki ya kuharibu miti na misitu bila hitaji halisi.

- Je, unaweza kukumbuka makosa yaliyofanywa katika eneo lako, ambazo baadaye zina maana chakula kidogo (au afya mbaya)?



SOMO LA BIBLIA 3

Kuzaa matunda kama wakristo

Soma Marko 11:12-14 na 11:20-21

Hadithi hii inaonyesha nje ya tabia kwa Yesu, kwa kawaida aliwatia moyo wengine hivyo inaonyesha kushangaza kwamba yeye alilaani mti huu, mti ulifunikwa na majani yenye afya, ambayo kwa kawaida yanazaliwa wakati mmoja kama matumba ya maua kutoka ambayo huwa tini baadaye. Matumba ya maua yanafanana na tini zilizoiva katika muonekano. Lakini Yesu hakuna matumba ya maua au matunda yaliyoiva – inapooza (ya majani peke yake).

- Je, Yesu alilaani mti kwa sababu alikuwa amechoka au alikuwa na njaa? Au je, alikuwa na sababu nyingine ya kufanya hivi?
- Je, Yesu alifundisha nini juu ya hitaji juu yetu kuzaa matunda?
- Je, aina ya matunda gani tunapaswa kuzaa kama wakristo?
- Je, ni kitu gani kinaweza kutupa mwonekano wa Mkristo halisi katika maisha – kama majani – bila kuzaa tunda lolote?
- Je, unafikiri alikuwa anamwambia nani hapa? Wanafunzi wake, umati au mamlaka za dini?

Huu ni mfano ambao unatupa sisi soma wazi katika kuhitaji kuhakikisha kwamba maisha yetu yasionekane, kama mazuri kutoka nje lakini yanazaa aina la tunda ambalo Yesu anataka kuona.

SOMO LA BIBLIA 4

Wajibu kwa mungu

Soma Kumbukumbu 6:4-5, Mwanzo 1:26 na 2:15 mistari hii yote inatufundisha kitu fulani juu ya wajibu wetu kwenye nchi na uumbaji wa Mungu.

- Jadili sehemu ambayo Mungu anatumaini tufanye. Je, hili linamaanisha nini katika maisha yetu kwa vitendo?
- Wakati gani sisi tunafanya kazi katika mashamba na bustani yetu, kuchunga wanyama wetu na kuwaangalia wagonjwa, kwa niaba ya nani tunafanya kazi kihalisi?
- Wakati watoto wetu au jamii zetu ni wagonjwa au wadhaifu kwa sababu hawajakula sawa sawa , je ni nani anayehusika?
- Kwa njia gani inawezekana kwa sisi kuharibu vitu ambavyo ni mali ya Mungu?

Jadili namna sisi tunaweza kufanya kazi pamoja kutunza uumbaji wa Mungu. Omba kwamba sisi tujifunze zaidi na zaidi kwa kufaa vile ina maana kuwa mawakili wahusika.

SOMO LA BIBLIA 5

Kujali/kutunza mazingira

Soma Mathayo 10:29 – 31

- Je, ndege wadogo ni muhimu kwa Mungu? Ndiyo! Anawalisha hao na hata kuivika mimea kwa maua mazuri (Mathayo 6:25 – 30). Lakini zaidi ya hayo, yeye huwajali/huwatunza watu. Sisi tuliumbwa kwa mfano wake, yeye anaweza kujua hata kama unywele mmoja umepotea! Hivyo wakati tunapaswa kutunza mazingira (na ndege na mimea) kwa sababu anavitunza, tungelitunza watu zaidi ya hivi.

- Je, kuna mabadiliko yoyote katika maeneo yetu ya jadi ambayo tungelifanya kwa sababu yatasaidia kwa uwazi watu wanaoishi hapo?

- Kama mabadiliko yamefanywa, je, kuna baadhi ya watu watapingana nayo kwa sababu mazingira (miti, wanyama, mito, nk) ni maalum zaidi kwao kuliko watu ambao wangefaidika? Je, unawezaje kutatua tatizo hili kwa ajili ya mema ya jumuia?

  Katika Biblia uumbaji wote ni muhimu sawa sawa na watu. Tuna maanisha kufanya kazi katika umoja pamoja na ulimwengu Mungu ameumba kutuunga mkono sisi. Jipe moyo wakati unataka kulinda mazingira na watu ambao wanaishi hapo. Mradi huu mgumu pia upo kwenye ajenda za Mungu (au kwenye orodha ya vitu vya Mungu vya kujadiliwa).

SOMO LA BIBLIA 6

Kuutunza uumbaji wenye manufaa

"Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi Matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Dunia imejaa mali zako". (Zaburi 104:24). Mungu anatutaka sisi kutuza uumbaji wenye manufaa.

Soma Ezekieli 34:17 – 19

- Je, aya hii afunua nini juu ya jinsi gani tungeli ushulikia uumbaji wa Mungu?

- Je, ni kwa jinsi gani tungefikiria mahitaji ya watu wengine na viumbe vingine? Kwa sababu Mungu alifanya vitu vyote na vinashika mana vyote kupita Yesu (Wakolosai 1:15 – 20), kila kitu ni mali yake wakati Mungu anatuongoza kwenye majani mabichi na maji safi (Zaburi 23), dunia ni mali ya Mungu peke yake (Zaburi 24:1), vyake ni karama sio vya kwetu. Vyake ni karama ambavyo sio lazima kuchukuliwa kutoka kwetu au viumbe vingine!.

- Je, tunafanya nini kutunza uumbaji na viumbe vya Mungu? Je, tunapinga tamaa ya kuwa wachoyo (Mathayo 6:33)?

- Je, tunatoa eneo (sehemu) kwa ajili ya maua na ndege katika ardhi yetu au katika jumuia zetu?

  Kutunza sehemu zetu kwa faida kwa ajili ya viumbe wote wa Mungu kunaleta sifa kwa Mungu, muumba na mmilikaji wa vitu vyote.

SOMO LA BIBLIA 7

Baba yetu mkulima

Tumejifunza katika mwongozo huu jinsi ya kusaidia miti michanga kukua vizuri – kwa kuiwekaea samadi, mboji au mbolea kama ikipandwa. Miti pia inaota vizuri na kuzaa matunda mengi katika mwanga wa jua wa kutosha. Hapa tunafikiri aina ya utunzaji na mafunzo tunayahitaji kama wakristo wenye kuzaa matunda mengi. Aya hii (ukurasa huu) inatoa taswira Mungu kama mkulima mwangalifu.

Soma Yohana 15:1 – 8.

- Yesu anatamani maisha yetu kuwa yenye kuzaa sana kwa ajili yake. Je, unakuwa katika mwanga wa kutosha wa jua la upendo wa Mungu? Tafakari juu ya maisha yako na kulinganisha kwenye ukuaji wa mzabibu au mti wa matunda.
- Je, umepandikizwa thabiti kwenye mzabibu ili uhai wake uweze kutililika katika wewe? Je, wewe unaangalia uhusiano wako na Yesu kupitia neno la Mungu, maombi na ibada na watu wake?
- Je, matunda ya aina gani tunazaa kwa ajili ya Mungu?
- Je, sisi tunahitaji Mungu kuondoa sehemu zozote za maisha yetu ili tuweze kuzaa zaidi matunda kwa ajili yake?

Katika mstari wa 15 Yesu anatuambia kwamba hatuwezi kufanya kitu pasipo yeye. Sisi tunaweza kuzaa matunda kama tunajaribu na kuwa kama yeye na kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote, roho zetu zote, akili zetu zote na nguvu zetu zote. Ufunguo hapa ni “yote” sio kidogo tu au nyingi lakini kwa “yote” wakati tunafanya hivi, kisha maisha yetu yataangaza kwa upendo wake kwa wengine na tutazaa matunda mengi kweli kweli.

SOMO LA BIBLIA 8

Hitaji/takwa letu na sio uchoyo wetu

Soma Mithali 30:7 – 9

Ni vizuri kukaa na kufikiri ni hali gani zinazotawala njia zote kwa kulima na maisha yetu.

- Je, nini ingekuwa hali zetu kile tunapata kutoka ardhi?
- Je, jinsi gani tungepaswa kuwatendea watu wengine, hasa wasio na kitu kuliko wenyewe?
- Jinsi gani sisi tunapaswa kuziona fedha?
- Je, ni nini sababu zetu za kutaka kustawisha maisha yetu na kilimo? Je, ni ili tu tuinue viwango vya maisha yetu – au ni ili tuweze kumsifu Mungu katika kila kitu ambacho tunacho?

Omba kwamba sisi tunajifunza kwa manufaa zaidi nini ina maanisha kuwa mawakili wanaowajibika.

SOMO LA BIBLIA 9

Miti kama picha ya imani

Soma Zaburi 1:1-5 na Yeremia 17:7-8

- Je, jinsi gani wakristo wanavyoweza kujilinganisha na miti? Je, milingano mingapi unaweza kupata katika hizi kurasa? Je, mistari hii inafundisha nini juu ya imani ya kikristo na nini inatokea katika nyakati ngumu?

- Je, umeona hili kuwa kweli katika maisha yako? Kama sio, kwa nini unafikiri hili kuwa hivyo?

Orodha ya majina kwa ajili ya miti mwitu muhimu

Jina la Kisayansi (Kitaalam)	Jina la Kawaida	Jina la Kiingereza/Biashara
Acacia auriculiformis	mkesia	Australian wattle, earleaf acacia, earpod black wattle
Acasia mearnsii	muwati	Australian acacia, black wattle, green wattle, late black wattle, tan wattle
Anacardium occidentale	mbibo, mkanju, mkorosho	cashew
Azadirachta indica	mkilifi, mwarubaini, mwarubaini kamili	neem
Balanites aegyptiaca	mkoga, mjunju, mwambangoma	desert date
Calliandra calothyrsus	mkaliandra	red calliandra
Cassia abbreviata	mbaraka, mkakatika	long pod cassia
Casuarina equisitofolia	moinga, mvinje	swamp she oak, whistling pine
Dovyalis caffra	mchongoma	Kei apple
Faidherbia albida	mgunga, mkababu	gao, white acacia, white-thorn, winter thorn
Gliricidia sepium		mother of cocoa, Mexican lilac, madre de cacao
Leuceana leucocephala	lusina, mlusina	Leuceana
Melia azedarach	mmelia, mwarubaini nusu	Melia, Persian Lilac
Moringa oleifera	mlonge, mronge, mrongo, mzunze	Moringa
Prosopis juliflora	mkikwa, kikwajukwaju	Mesquite
Sesbania macrantha	mlindaziwa	Sesbania
Tamarindus indica	mkwaju, msisi	Tamarind



Kilimo Mseto

Mwongozo wa nguzo

Na Isabel Carter

Tafsiri na Arthur Mbumbuka, PO Box 2529, Mbeya, Tanzania
Barua-pepe: **mbumbuka@excite.com**

Published by Tearfund
100 Church Road, Teddington, TW11 8QE, UK
Registered Charity No 265464